UNICEF Innocenti – Ofisi ya Kimataifa ya Utafiti na Utabiri

unicef | for every child

MUHTASARI WA SERA



© UNICEF/UNI94707/NOORANI

# Ujana Salama: Mpango wa Nyogeza ya Ruzuku Unaohusu Mabadiliko Salama kutoka Ujanani hadi Utu Uzima wenye Afya na Ustawi

Matokeo ya Awamu ya 4

## Utangulizi

Ujana Salama ('Safe Youth' kwa Kiingereza), mpango wa Ujana Salama Nyongeza ya Ruzuku (' Ujana Salama-Cash Plus') unaohusu mabadiliko salama kutoka ujanani hadi utu uzima wenye afya na ustawi, ni mradi wa majaribio jumuishi ya kinga ya jamii ambao unalenga kuboresha

fursa za kiuchumi za baadaye za vijana na kuwezesha mabadiliko salama na yenye afya kuelekea utu uzima na wakati huo huo kuimarisha uwezo wa serikali za mitaa wa kupanga na kutekeleza huduma zinazohusiana na afya ya vijana, stadi za kazi na kinga ya jamii. Vijana wengi Katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wanakabiliwa na hatari nyingi za kiafya na kiuchumi, ikijumuisha umaskini, fursa ndogo za ajira rasmi, kukatisha masomo mimba za mapema, magonjwa ya zinaa, ukatili, unyanyasaji na unyonyaji, ambavyo vinaweza kuzuia ustawi wao na fursa za baadaye.[1]

Mradi wa Ujana Salama unatekelezwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii Tanzania (TASAF) na kuendeshwa kupitia Mpango wa Serikali ya Tanzania wa Kunusuru Kaya Maskini (PSSN), mpango wa kinga ya jamii unaojumuisha utoaji wa ruzuku, ajira za muda na mpango wa kukuza uchumi wa kaya na kuwekeza unaofikia kaya zaidi ya milioni moja kitaifa. Ujana Salama hulenga vijana katika kaya ambazo tayari zinapokea ruzuku kupitia Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini na hujumuisha huduma za mafunzo na ushauri nasaha, ikitilia mkazo stadi za kazi na afya ya uzazi na ujinsia. Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto Ulimwenguni (UNICEF) na Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (TACAIDS) walitoa msaada wa kiufundi kwa mpango wa Ujana Salama. Mradi wa majaribio wa Ujana Salama ulitekelezwa kwa mara ya kwanza katika mikoa ya Mbeya na Iringa na baadaye ulipelekwa katika mikoa ya Kigoma na Songwe. UNICEF Innocenti - Ofisi ya Kimataifa ya Utafiti na Utabiri (UNICEF Innocenti), Chuo Kikuu cha Buffalo (Chuo Kikuu cha Jimbo la New York) na EDI Global ilitumia njia mchanganyiko za kitafiti zinazotumia muda mrefu katika kutathmini na kupima matokeo (kilongitudo) ya mradi kwa kushirikiana na TASAF, TACAIDS na UNICEF Tanzania.[2]

Tathmini ya matokeo ya mradi ilijumuisha awamu nne za ukusanyaji wa takwimu kati ya mwaka 2017 na 2021. Awamu mbili za kwanza za ufuatiliaji (2018 na 2019) zilitathmini na kupima matokeo yaliyoainishwa kijinsia, pamoja na matokeo yanayohusiana na jinsia kama vile ukatili, mitazamo ya kijinsia, ufikiaji wa huduma za Afya ya uzazi na ujinsia, ujauzito na ndoa.[3] Hata hivyo, maswali yalibaki kuhusu athari za muda mrefu za mpango wa majaribio wa Ujana Salama kwa usawa wa kijinsia, mchango wa utekelezaji katika kushawishi matokeo ya usawa wa kijinsia na jinsi changamoto za utekelezaji (hasa, ucheleweshaji wa malipo ya ruzuku) zilivyoathiri mikakati ya kijinsia ya kukabiliana na hali husika.

Muhtasari huu umejikita katika matokeo ya tathmini ya Awamu ya nne (4). Tathmini hii ya athari katika awamu ya ufuatiliaji ya 2021, ikijumuisha matokeo ya usawa wa kijinsia kama sehemu ya mpango mpana wa Utafiti wa kinga ya jamii unaozingatia Mwitikio wa Kijinsia na Umri (GRASSP) (2018-2023), unaoongozwa na UNICEF Innocenti na kufadhiliwa na Ofisi ya Mambo ya Nje, Jumuiya ya Madola na Maendeleo ya Serikali ya Uingireza na Ireland Kaskazini (FCDO).

Vijana wanakabiliwa na hatari na vitisho vingi vya kijinsia katika ustawi na afya zao. Kwa kutambua hatari hizi, mpango wa Ujana Salama hutumia mbinu ya kuimarisha uwezo, kuwapa vijana mchanganyiko wa mtaji wa kijamii, kiafya na kifedha ambao hupanua uwezo wao wa kufikia kile wanachotaka "kuwa au kufanya."[4] Kinga ya jamii imeonesha kuboresha matokeo yanayohusiana na mabadiliko salama ya ujana kuingia utu uzima; hata hivyo, fedha pekee hazitoshi kuleta ulinzi au mabadiliko husika (yaani, kuboresha kipato na uwezo au kuboresha usawa wa kijamii na ujumuishaji).[5] Hivyo basi, kuchanganya uwezeshaji wa kifedha, kuwa na programu za ziada na kuoanisha na huduma zilizopo (ambazo mara nyingi hujulikana kama Nyongeza ya Ruzuku), pamoja na kuunganisha mambo yanayohusiana na jinsia katika kuunda programu, kunaweza kuboresha matokeo ya fedha na kuleta mabadiliko chanya. Mpango wa Ujana Salama huchagiza uwezekano wa Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini kuleta matokeo chanya kupitia programu za ziada zinazozingatia jinsia.

Programu hii na tathmini ya athari inaendana na mfumo dhana na ushahidi kutoka katika programu ya utafiti ya GRASSP.[6] Vipengele vya programu ya Ujana Salama ikijumuisha mafunzo ya stadi za kazi, afya ya uzazi na ujinsia, na mitazamo ya kijinsia, vinaweza kuboresha matokeo ya usawa wa kijinsia, na ni hatua muhimu katika kukuza "mifumo ya kinga ya kijamii inayozingatia jinsia" na umri, yakilenga kuwezesha mabadiliko salama ya kutoka ujanani kwenda utu uzima.

Programu pia ina uwezo wa kutatua mahitaji maalum ya kijinsia na kuimarisha uwezeshaji wa wasichana na wanawake kupitia njia za kawaida kama vile uwekezaji katika maendeleo ya binadamu, uhuru na kujiamini, kuimarisha utoaji wa huduma zinazozingatia jinsia, kuboresha mitazamo ya usawa wa kijinsia kuhusu huduma zisizokuwa na malipo na kazi za nyumbani, na kuongeza ushiriki wa wasichana katika kazi.

Zaidi, Awamu ya 4 ya tathmini ya athari ilichunguza mchango wa vipengele vinavyoshawishi matokeo kama vile tamaduni za kijamii na kijinsia ambazo zinaweza kuwa vichochezi vya kimuundo vya matokeo ya usawa wa kijinsia.

## Ujana Salama: Mpango wa Ujana Salama

Ujana Salama ulilenga vijana wenye umri wa miaka 14–19 (kwa kuanzia) katika kaya za Walengwa wa Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini na ulikuwa na nyanja tatu:

- Kutoa mafunzo kuhusu afya ya uzazi na ujinsia na stadi za maisha za VVU, ikijumuisha mitazamo na tamaduni za kijinsia (*tazama mada katika Sanduku la 1*)
- Ushauri (kuhusu chaguzi za stadi za kazi na masuala ya maisha) na ruzuku zenye tija kwa ajili ya elimu, mafunzo ya ufundi au mipango ya biashara
- Kuimarisha vituo vya afya pamoja na kuwapo kwa huduma za kiurafiki kwa vijana za VVU, afya ya uzazi na ujinsia na kukabiliana na ukatili

Maeneo manne ya mamlaka ya miradi ya TASAF yalichaguliwa kutekeleza programu ya Ujana Salama, kwa kuzingatia muingiliano kati ya vipaumbele vya TASAF na mikoa ambayo UNICEF ilikuwa ikisaidia programu zilizopo.[7] Maeneo husika ni Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi na Halmashauri ya Mji wa Mafinga huko Iringa, na Wilaya ya Rungwe na Busokelo huko Mbeya.

Ratiba ya utekelezaji wa mradi/mpango ulikuwa kama inavyoonekana katika mchoro hapo chini (tazama Kielelezo Na. 1).

**SANDUKU NA. 1.**
**MADA ZA MAFUNZO**


**Stadi za kazi**

- Ndoto na malengo
- Stadi za ujasiriamali
- Mipango ya biashara na kuweka rekodi
- Kuweka akiba

**VVU & Afya ya Uzazi na Ujinsia (SRH)**

- Kukabiliana na balehe
- Mahusiano
- Elimu ya Virusi Vya Ukimwi (VVU), kinga na kujilinda
- Tabia hatarishi za ngono na kujilinda
- Mimba na uzazi wa mpango
- Ukatili na ukatili wa kijinsia
- Kukabiliana na mitazamo na tamaduni hasi za kijinsia

**Kielelezo Na 1. Ratiba ya utekelezaji wa mradi**




## Tathmini

Utafiti huu ulitumia washiriki (sampuli) waliopatikana kwa njia ya Bahati nasibu inayodhibitiwa na jamii husika muundo wa utafiti wa cRCT, ambapo vijiji (jopo la sampuli) 130 viligawanywa bila mpangilio katika sehemu mbili za utafiti:

1. Vijiji vya majaribio (mradi): vijiji vyenye mradi wa Ujana Salama ambapo fedha zaidi ilitolewa kama nyongeza kwa kaya ambazo tayari zinapokea fedha za ruzuku kutoka katika Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini ikiwa ni pamoja na Ujana Salama

2. Vijiji vya ulinganifu (uangalizi): vijiji vinavyopokea fedha za Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini tu

Huu ni utafiti unaotumia njia mchanganyiko ya kilongitudo, unaojumuisha utafiti wa awali (2017), Awamu ya 2 (2018), Awamu ya 3 (2019) na Awamu ya 4 (2021).[8] Utafiti ulihusisha vituo vya afya, viongozi wa kijamii, wakuu wa kaya na vijana.

Tathmini iliangazia athari za mradi wa Ujana Salama kwa ustawi wa vijana kuelekea utu uzima uliojumuishwa katika muundo wa mpango wa serikali wa uhawilishaji fedha. Matokeo muhimu ya mpango huu ni pamoja na uhakika wa stadi za kazi na kiuchumi; kuchelewa kujiingiza katika ngono, ndoa, na kupata ujauzito; kupungua kwa uwezekano wa kufanyiwa ukatili; na kuimarika kwa afya ya akili (*tazama Sanduku la 2*).

Muhtasari huu unaangazia matokeo ya awamu ya nne (4) ya ukusanyaji takwimu, uliofanywa kati ya Januari  na Machi 2021, miezi 18–20 baada ya kipindi cha mwisho cha programu na miezi 32 baada ya kipindi kirefu cha programu. Awamu ya 4 ilitathmini uwezekano wa matokeo husika kuendelezwa baada ya utekelezaji wa programu kufika mwisho.

Kwa kuongezea, ilishughulikia maswali ya utafiti yafuatayo kuhusu matokeo ya usawa wa kijinsia:

- Je, matokeo ya muda mrefu yana ujinsia (ndani ya miaka miwili baada ya kukamilika kwa shughuli za mwisho za mradi wa majaribio) katika mpango wa Ujana Salama unaotekelezwa kama sehemu ya programu inayolenga vijana?
- Jinsi gani mikakati ya kukabiliana na ucheleshwaji wa ruzuku za kaya  kati ya 2019 na 2020 hutofautiana kati ya wavulana na wasichana?
- Utekelezaji wa mpango wa Ujana Salama umeathiri vipi matokeo ya usawa wa kijinsia?
- Ni jinsi gani sababu za kimazingira (kama vile, mila na desturi na mitazamo kuhusu jinsia , upatikanaji wa soko, ubora na umbali wa vituo vya afya) huathiri matokeo ya programu?

**SANDUKU NA. 2.**
**MATOKEO YA TATHMINI**

### Matokeo ya muda mfupi

- Matarajio ya kielimu na kikazi
- Mitazamo sahihi ya usawa wa kijinsia
- Ujuzi wa njia za kisasa za uzazi wa mpango
- Ujuzi wa kuzuia VVU
- Ujuzi wa wapi pa kupata huduma za Afya ya Uzazi na Ujinsia (SRH)/ VVU na kukabili ukatili

### Matokeo ya kati na muda mrefu

- Fursa za ajira kwa vijana na mipango ya kujiongezea kipato
- Kupata elimu na mafunzo
- Kuongezeka kwa uwezo wa kutafuta huduma sahihi za afya ya uzazi na ujinsia /VVU na kukabiliana na ukatili
- Kuchelewa kuanza kufanya ngono, kuolewa na ujauzito
- Kupunguza ushiriki katika ngono za kinyonyaji na tabia hatarishi za VVU
- Kuboresha afya ya akili
- Kupunguza nafasi ya kuwa mhanga wa ukatili

Maswali ya vijana yanayozingatia idadi/wingi yalishughulikia mada kadhaa na yalijikita kwenye nadharia ya mabadiliko ya programu, kama ilivyoelezewa katika ripoti ya awali.[9] Waligusia matokeo ya kati (maarifa, mitazamo na matarajio) na matokeo ya kati na muda mrefu (mabadiliko ya tabia na matumizi ya huduma za afya).

Sehemu mbili za utafiti ziliwahoji vijana katika awamu zote za utafiti. Sampuli ya msingi ilijumuisha vijana 2,458 wenye umri wa miaka 14–19. Kati yao, 2,104 (asilimia 86) walihojiwa tena katika tathmini ya kati, 2,191 (asilimia 89) walihojiwa tena katika Awamu ya 3, na 2,053 (asilimia 84) walihojiwa tena katika Awamu ya 4. Muhtasari huu unajikita kwenye matokeo yatokanayo na takwimu zilizokusanywa kwa vijana ambao walihojiwa awali na katika Awamu ya 4 – sampuli ya paneli.[10]

Katika upembuzi unaozingatia kiasi/kiwango, tulitumia takwimu kutoka katika sampuli ya paneli ya vijana katika vijiji vya majaribio na ulinganifu na kulinganisha mabadiliko kati ya vikundi hivi viwili kwa muda.[11] Kwenye upembuzi unaozingatia ubora, tulichunguza namna na njia za matokeo kwa kufanya mahojiano ya kina na sampuli ya vijana 32 katika Awamu ya 4. Mahojiano ya ziada ya ubora na walengwa wa programu, watekelezaji na watoa taarifa muhimu yalituruhusu kuchambua vipengele vya usawa wa kijinsia kuhusiana na utekelezaji wa programu.

## Tafasiri

Wakati wa kutafasiri matokeo ya Awamu ya 4, kuna mambo kadhaa ya kuzingatia. Kwanza, tulikadiria athari kwa takriban miezi 20 baada ya programu ya Ujana Salama kufika mwisho. Tulizingatia athari kwenye anwai ya matokeo ya afya ya uzazi na ujinsia, bila kujali kama mpango (mradi) uliathiri matokeo haya katika awamu za awali za tathmini. Kuna uwezekano kwamba ingawa athari zingine zilijitokeza wakati huu, zingine zilitoweka baada ya kumalizika kwa programu. Pili, kaya zilichelewa kulipwa kwa jumla ya miezi 18 baada ya Machi 2019, ambayo huenda ilidhoofisha baadhi ya matokeo chanya ya mpango wa Ujana Salama yaliyoonekana katika tathmini zilizotangulia. Tatu, janga la UVIKO-19 lilisababisha athari mbaya za kiuchumi ambazo zinaweza kuathiri faida za mpango wa Ujana Salama. Nne, kutokana na matokeo mbalimbali yaliyotathminiwa katika tathmini hii ya athari, hatukutarajia athari kubwa za programu kwenye matokeo yote.

Muhtasari huu unaangazia athari za programu kwenye viashiria mbalimbali katika awamu zilizopita na kama athari hizi ziliendelea kujionyesha katika Awamu ya 4. Tathmini iligundua kuwa mpango uliboresha maisha ya vijana wanaoshiriki katika nyanja nyingi. Athari zimefupishwa (tazama *Jedwali Na. 1*) na kujadiliwa kwa undani zaidi hapa chini. Muhtasari pia unajadili uchambuzi wa kina wa usawa wa kijinsia, ikiwa ni pamoja na jinsi matokeo yalivyotofautiana kati ya wavulana na wasichana, pamoja na ambavyo viwango vya utekelezaji vilivyochangia matokeo husika.

**Jedwali Na. 1. Muhtasari wa athari za programu katika awamu zote kwenye viashiria vilivyochaguliwa**

| KIASHIRIA | AWAMU YA 2 | AWAMU YA 3 | AWAMU YA 4 |
|---|---|---|---|
| Kushiriki katika shughuli zozote za kiuchumi wiki moja kabla ya mahojiano | ↑↑ | | ↑ |
| Muda unaotumika katika shughuli za kiuchumi | | | ↑↑ |
| Ana biashara | Haijatathminiwa | ↑↑↑ | ↑↑ |
| Anamiliki mifugo | Haijatathminiwa | ↑↑↑ | ↑↑↑ |
| Ufugaji wa mifugo | ↑↑↑ | ↑↑ | ↑↑ |
| Kushiriki katika kazi zozote za nyumbani siku moja kabla ya mahojiano | | | |
| Anahudhuria shule | | ↓↓ | |
| Kujithamini au kujisimamia | | ↑↑ | |
| Maarifa kuhusu VVU | ↑↑ | ↑↑ | |
| Upimaji wa VVU | | ↑↑ | |
| Maarifa ya uzazi wa mpango | ↑↑ | ↑↑ | |
| Kutumia uzazi wa mpango | | | |
| Kufuatilia afya ya ujinsia na uzazi | | ↑ | ↑ |
| Kushiriki ngono mara ya kwanza | | | |
| Ndoa au kuishi pamoja | | ↑ | ↑ |
| Tofauti kubwa ya umri katika mahusiano au biashara ya ngono | | | |
| Matumizi ya kondomu mara ya mwisho uliposhiriki ngono | | | |
| Mitazamo sahihi ya usawa wa kijinsia | ↑↑ | ↑↑ | |
| Dalili za sonona | | ↓↓↓ | ↑ |
| Kukumbwa na ukatili | | ↓↓ ↓ | ↓ |
| Kufanya ukatili | Haijatathminiwa | ↓↓ | |

Maelezo: ↓ inahusu kupungua kwa matokeo na ↑ inaonesha kuongezeka kwa matokeo. Mshale mweusi unarejelea athari katika sampuli jumuishi (wavulana na wasichana), mshale wa zambarau unarejelea sampuli ndogo ya mwanamke na mshale wa kijani unarejelea sampuli ndogo ya mwanamume; masanduku matupu hayaoneshi athari isipokuwa kama imebainishwa vinginevyo. Uwezo wa kujisimamia hupima kiwango ambacho vijana wanaamini kuwa wana udhibiti juu ya matokeo au matukio katika maisha yao, kinyume na nguvu za nje zinazodhibiti maamuzi yao.

## Matokeo ya Awamu ya 2

Ripoti ya Awamu ya 2 ya utafiti inaonesha kuwa, wakati wa tathmini ya kati (2018), baada ya vijana kupata mafunzo ya ana kwa ana ya wiki 12, kulikuwa na athari chanya katika ushiriki katika shughuli za kiuchumi, mitazamo ya usawa wa kijinsia, na maarifa yanayohusiana na VVU na afya ya uzazi na ujinsia.[12] Lakini, hakukuwa na athari juu ya ukatili, tabia hatarishi za VVU au kuboreka kwa tabia ya kujielimisha kuhusu afya ya uzazi na ujinsia na VVU. Matokeo haya yanasisitiza jinsi, wakati na mara baada ya mafunzo, vijana wanaweza kuwa wameanza kupata maarifa mapya na kufikiria juu ya mustakabali wao kwa njia tofauti. Lakini, kufikia Awamu ya 2, walikuwa na muda mfupi tokea waanze programu na vipengele vingine (ushauri, misaada yenye tija na uimarishaji wa upande wa usambazaji) vilikuwa bado havijaanza. Ilidhaniwa kwamba matokeo haya ya kitabia yangechukua muda zaidi kuonekana na huenda yangeonekana wakati wa Awamu ya 3 ikiwa, kwa kweli, mpango huo ungeathiri matokeo haya.

## Matokeo ya Awamu ya 3

Kama ilivyodhaniwa hapo juu, Matokeo ya Awamu ya 3 (2019) yalionesha kuongezeka kwa utoaji wa huduma za kirafiki kwa vijana katika vituo vya afya, pamoja na athari chanya katika: afya ya uzazi na ujinsia (SRH) na maarifa ya VVU; mitazamo inayofaa ya kijinsia; uwezekano wa kuanzisha biashara; masaa yaliyotumika kutunza mifugo; afya ya akili; mitazamo ya kijasiriamali; kujithamini; kupima VVU; na kutembelea vituo vya afya. Athari za ziada za kinga zilionekana, ikijumuisha kupungua kwa matukio ya ukatili wa kingono na unyanyasaji wa kimwili. Hata hivyo, tulibaini pia kupungua kwa mahudhurio ya shule za sekondari miongoni mwa vijana wa kike wenye umri mkubwa.[13]

## Matokeo ya Awamu ya 4

Katika Awamu ya 4 (2021), tulipata matokeo kadhaa endelevu ya mpango wa Ujana Salama. Hata hivyo, baadhi ya matokeo yaliyopatikana hapo awali katika Awamu ya 2 na 3 hayakudumishwa, labda kwa sababu ya matukio kadhaa mabaya (kwa mfano, UVIKO-19 na ucheleweshaji wa malipo ya ruzuku kwa  Walengwa wa Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini) yaliyowakumba vijana na wengine katika kaya zao katikati ya awamu. Tunatoa muhtasari wa matokeo kulingana na eneo husika hapa chini.

### Elimu na ushiriki kiuchumi

- Mpango wa Ujana Salama ulikuwa na athari endelevu kwa shughuli ndogo ndogo za ujasiriamali za vijana. Kama ilivyo katika Awamu ya 3, vijana katika vijiji vya majaribio walikuwa na uwezekano mkubwa wa kuendesha biashara kuliko vijana katika vijiji vya ulinganifu (wakati wa tathmini ya kati, hakuna athari zilizoonekana) na mapato yaliongezeka kutokana na programu.

- Miongoni mwa wasichana, programu ilisababisha ushiriki mkubwa katika baadhi ya shughuli maalum za kiuchumi ikiwa ni pamoja na ufugaji na kazi za shamba.

- Kutokana na ushiriki mkubwa katika shughuli za kiuchumi na shughuli ndogo ndogo za ujasiriamali, uwezekano wa kupata ajali kazini uliongezeka kutokana na mradi katika Awamu ya 4 (hii haikuonekana katika awamu zilizopita).

- Wasichana katika vijiji vya majaribio ya mpango wa Ujana Salama walitumia muda mwingi kuwatunza wazee au wagonjwa ikilinganishwa na wenzao katika vijiji vya ulinganifu. Kufuatia programu hiyo, uwezekano wa wasichana kuokota kuni pia uliongezeka. Hakukuwa na athari katika kazi zingine za nyumbani. Ushiriki wa jumla katika kazi zozote za nyumbani haukuathiriwa.

- Wakati katika Awamu ya 3 kulikuwa na ongezeko la kuacha shule kwa wasichana kutokana na mradi, kufikia Awamu ya 4 athari hii isiyotarajiwa haikuonekana tena, kwani wakati huo, vijana wengi walikuwa wameacha kabisa shule katika vijiji vya majaribio na ulinganifu. Kama ilivyokuwa katika awamu zilizopita, hakukuwa na athari za kielimu, inayotambulika kama daraja la juu la elimu iliyofikiwa. Kwa hivyo, athari hasi za mahudhurio shuleni zilizoonekana katika Awamu ya 3 hazikuweza kuwa matokeo endelevu ama kuwa athari hasi kwa vijana wanaoshiriki katika mpango wa Ujana Salama kupata elimu.

## Mtazamo, hatari na usaidizi wa kijamii

- Katika awamu ya tatu, athari chanya za programu juu ya kujithamini zilionekana, lakini hizi hazikuonekana katika awamu ya nne, wakati kujithamini kulikuwa kumeongezeka katika vijiji vyote vya majaribio na ulinganifu. Matokeo hayo hayo ya programu yalijitokeza kwenye mitazamo ya ujasiriamali.

- Kama ilivyonekana katika Awamu ya 2 na 3, kwenye Awamu ya 4 programu haikuwa na athari kwenye msaada wa kijamii, ustawi binafsi au ufanyaji maamuzi miongoni mwa vijana.

## VVU, afya ya uzazi na ujinsia (SRH) na kuunganishwa kwenye huduma

- Kama yalivyo matokeo katika Awamu ya 3, kulikuwa na athari endelevu za programu juu ya matumizi ya huduma za afya kwa wavulana.

- Wakati mpango uliongeza maarifa juu ya dawa za uzazi wa mpango katika awamu zilizopita, kufikia Awamu ya 4 athari hazikuendelezwa kwani makundi yote ya majaribio na ulinganifu yalikuwa na viwango vya juu vya maarifa.

- Sawa na awamu tangulizi, matumizi ya dawa za uzazi wa mpango hayakuathiriwa na mpango wa Ujana Salama

- Mpango wa Ujana Salama uliongeza uwezekano wa vijana kujua kwamba wanaweza kufanya uzazi wa mpango na kupima ujauzito katika zahanati, na matokeo haya yalichochewa na sampuli ya wasichana.

- Kufikia Awamu ya 4, athari chanya za programu juu ya maarifa na kupima VVU yaliyopatikana katika Raundi ya 3 hayakuendelezwa. Hii inaweza kusababishwa na kushamiri kwa ujuzi juu ya VVU katika kikundi shiriki na wenzao, pamoja na vijana kuwa watu wazima na kuwa na ujuzi zaidi kuhusu afya ya uzazi na ujinsia kwa ujumla. Viwango vya upimaji wa VVU viliongezeka baada ya muda. Hata hivyo, matokeo ya awali ya mpango kwenye matokeo haya yanaweza kuboresha afya ya vijana katika siku zijazo.

- Kufikia Awamu ya 4, mpango wa Ujana Salama uliongeza uwezekano wa vijana kuripoti kutokuwa na hatari ya VVU ikilinganishwa na hatari ya chini, wastani au juu.

- Ingawa mpango wa Ujana Salama haukuathiri hali ya wasichana wanaoshiriki katika programu kuhusu ujauzito, iliongeza uwezekano wa wasichana wenye wapenzi wa kiume kuwa wajawazito, labda kwa sababu ya kuongezeka kwa viwango vya kuoa miongoni mwa wavulana kufuatia programu. Kutokana na kuongezeka kwa utulivu unaotolewa na mradi wa Ujana Salama, washiriki wanaweza kuwa wamejiandaa vizuri zaidi kujenga na kutunza familia zao wenyewe.

- Programu haikuwa na athari kwenye ndoa au kuishi pamoja, kulazimishwa kufanya ngono kwa mara ya kwanza, uhusiano baina ya watu wanaopishana sana umri, kuanza ngono au kufanya ngono ya kibiashara . Uchambuzi kwa sampuli ndogo unaonesha kuongezeka kwa ndoa au kuishi pamoja kwenye sampuli ndogo ya wavulana.

## Kupunguza ukatili

- Kwa wasichana, programu ilipunguza hatari ya kukumbwa na  unyanyasaji wa kingono.

- Hakuna athari za programu zilizoonekana juu ya unyanyasaji wa kihisia, kimwili au ukatili baina ya wapenzi.

- Programu iliongeza uwezekano wa wavulana kutafuta msaada kutoka vyombo rasmi wakumbanapo na ukatili.

- Hakukuwa na athari katika vitendo vya unyanyasaji wa kihisia, na kupungua kwa vitendo vya ukatili wa kimwili miongoni mwa wavulana katika Awamu ya 3 haukuendelezwa katika Awamu ya 4.

## Afya ya akili

- Wakati kupungua kwa dalili za msongo wa mawazo kulihusishwa na programu katika Awamu ya 3, programu ilisababisha kuongezeka kwa dalili za msongo wa mawazo katika Awamu ya 4. Ikiwa programu iliongeza matarajio ya kazi na ustawi – na kusababisha afya bora ya akili katika Awamu ya 3 – vikwazo vilivyojitokeza katika janga la Korona vinaweza kuwa vimeathiri vijana katika vijiji vya majaribio kuliko wale walio katika vijiji vya ulinganifu.

- Hakukuwa na athari za programu kwenye viwango vya mfadhaiko.

## Kinga ya kijamii inayojali jinsia

Sehemu hii inaelezea kwa ufupi kuhusu matokeo yanayohusiana na jinsia, hasa athari za muda mrefu kuhusu matokeo ya usawa wa kijinsia, majibu ya ucheleweshaji wa malipo ya ruzuku za PSSN kulingana na jinsia, na mchango wa utekelezaji na sababu za kimazingira katika kuleta matokeo chanya ya usawa wa kijinsia.

- Athari za muda mrefu kwenye matokeo ya usawa wa kijinsia

    - Athari za programu juu ya mitazamo inayofaa ya kijinsia iliyobainishwa katika Awamu ya 2 na 3 hazikuonekana katika Awamu ya 4.

    - Kulikuwa na athari endelevu na chanya katika maeneo ya afya na kiuchumi, ambayo yanaweza kusababisha mabadiliko ya kinga ya jamii, kama vile wasichana kuendesha biashara, umiliki wa mifugo kwa wavulana na wasichana, wavulana kutumia huduma za afya, wasichana kuelewa wapi pakupata huduma za uzazi wa mpango na kupima ujauzito, na kupungua kwa wasichana wanaokumbwa na ukatili wa kijinsia.

    - Katika kaya zilizoshiriki, athari za mifumo ya matumizi ya muda ziliendelea kuwa za kijinsia, huku ongezeko lililochochewa na programu katika ufugaji na kazi za shambani zikizingatiwa miongoni mwa wasichana pekee.

    - Athari mpya katika awamu ya 4 ni pamoja na ongezeko la kazi ya kuhudumia (wagonjwa na wazee) miongoni mwa wasichana na kuongezeka kwa uwezekano mkubwa wa wavulana kutoa taarifa mwenzi wao wakiwa wajawazito.

- Athari za kijinsia juu ya ucheleweshaji wa malipo ya ruzuku kwa kaya zilizo katika Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini

    - Ili kukabiliana na ucheleweshaji wa malipo ya ruzuku kwa kaya zilizo katika Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini, kaya zilipunguza matumizi yao ya chakula na idadi ya milo wanayopata kwa siku, ziliingia kwenye madeni zaidi, ziliuza mali kama vile mifugo, zilijihusisha zaidi na vibarua, zilipunguza matumizi yao ya huduma za afya na ununuzi wa dawa, na kupunguza uwekezaji wao katika biashara ndogo ndogo; mahudhurio ya shuleni pia yaliathiriwa.

    - Mikakati hii ya kukabiliana na hali husika haikuonekana kuwa na ujinsia; wala ucheleweshaji wa malipo haukuzidisha ukosefu wa usawa wa kijinsia uliopo.

- Utekelezaji na ushawishi wake juu ya usawa wa kijinsia

    - Sababu muhimu katika kufikia matokeo anwai ya usawa wa kijinsia ni pamoja na vikao vya mradi vya kupeana taarifa, uajiri unaozingatia jinsia wa washauri na waelimishaji rika, na kuendesha mafunzo katika madarasa yenye jinsia mchanganyiko.

    - Vipengele kama vile ruzuku yenye tija ziliwajenga wasichana kiuchumi na kuboresha nafasi yao kijamii na kujiamini ili kuepuka tabia hatarishi za kingono.

    - Mapungufu katika mfumo wa utoaji taarifa katika jamii hizi yalibainishwa kama sababu ambayo iliwazuia waathirika wa ukatili kutoa taarifa au kutafuta msaada rasmi.

- Kudhibiti athari za sababu za kimazingira

    - Tamaduni za kijinsia na ufikiaji wa huduma zilikuwa na nafasi ndogo katika kudhibiti athari za programu, isipokuwa katika baadhi ya mambo.

    - Katika jamii zenye uhafidhina kuhusu matumizi ya uzazi wa mpango, programu ilipelekea viwango vya chini vya matumizi ya uzazi wa mpango, wakati katika jamii ambazo zinafuata usasa, mradi haukuathiri matokeo haya. Kwa kuongezea, tamaduni zenye usasa kuhusu masharti ya wasichana kufanya maamuzi, ziliwezesha mradi kuwa na ufanisi zaidi katika kuchelewesha kuanza ngono.

    - Wakati huo huo, inaonekana kwamba mradi ulisababisha kuongezeka kwa tabia za kutafuta huduma ya afya miongoni mwa vijana katika jamii ambazo zilikuwa na ufikiaji duni wa huduma bora za afya, ikionesha jinsi taarifa na mtandao wa huduma

unavyoweza kuboresha baadhi ya matokeo na kushughulikia mapungufu kadhaa katika upatikanaji huduma katika jamii zilizosahaulika.

## Hitimisho

Mpango wa Ujana Salama ulilenga kuongeza matokeo chanya za mpango wa Ujana Salama kwa kutoa mafunzo kwa vijana kuhusu stadi za kazi, afya ya uzazi na ujinsia (SRH) na VVU, ushauri na misaada yenye tija, pamoja na kuwaunganisha na huduma kirafiki za afya ya uzazi na ujinsia (SRH) na VVU. Programu hii ilikuwa ya kipekee, na yenye kugusa sekta mbalimbali, inayotekelezwa na serikali iliyolenga vijana walio kwenye mazingira magumu na kaya masikini wanaoshiriki katika mpango wa serikali wa kinga ya jamii. Programu ya Ujana Salama, wakati huo huo, iliboresha afya na uchumi wa vijana. Programu ilianza 2018–2019 na ilitathminiwa kwa kutumia njia mchanganyiko ya kilongitudo ya kupima athari kutoka 2017 (awali) hadi 2021 (Awamu ya 4).

Wakati wa tathmini ya kati, mara tu baada ya mafunzo ya stadi za kazi,  afya ya uzazi na ujinsia (SRH), tuliona athari chanya kwenye viashiria vya muda mfupi, kama vile maarifa ya afya ya uzazi na ujinsia (SRH), mitazamo chanya kijinsia na ushiriki katika shughuli za kiuchumi. Katika Awamu ya 3, tuliona baadhi ya mabadiliko katika tabia, ikiwa ni pamoja na: kuongezeka kwa upimaji wa VVU na kutembelea vituo vya afya; kuchelewa kuanza ngono; kupungua kwa ufanyaji au kufanyiwa ukatili; kuongezeka kwa mitazamo ya kujiamini na ujasiriamali; na kupungua kwa dalili za msongo wa mawazo . Baadhi ya mambo hayakubadilika na yalikuwa na athari hasi katika mahudhurio mashuleni, mwenendo ambao haukuendelea baadaye.

Katika Awamu ya 4, tulipata athari endelevu na chanya kwenye shughuli za kiuchumi, kuendesha biashara, ufugaji wa mifugo na wavulana kutumia huduma za afya. Mpango huu uliendelea kupunguza hatari ya wasichana kupatwa na ukatili wa kijinsia.

Mambo mawili muhimu yanaweza kuwa yamechangia kupunguza athari za mpango huu katika Awamu ya 3 na 4. Hizi ni pamoja na ucheleweshaji wa malipo ya ruzuku kwa kaya za Walengwa wa Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini (kati ya Machi 2019 na Septemba 2020) na janga la UVIKO-19 (kuanzia Machi 2020 hadi ukusanyaji wa takwimu katika Awamu ya 4, Januari-Machi 2021). Athari hizi mbaya za kipato kwa kaya zilihitaji vijana wanaoshiriki na kaya zao kuelekeza rasilimali zao kwenye chakula na mahitaji mengine ya msingi. Bila matukio haya, wangeweza kuelekeza rasilimali nyingi katika elimu, biashara au kwenye matokeo yanayohusiana na afya, kukoleza zaidi athari chanya za programu.

Ukosefu wa matokeo endelevu kuhusu afya ya akili na mitazamo chanya kijinsia inaonesha kwamba programu inapaswa kutekelezwa kwa muda mrefu au kwa kuhusisha shughuli nyingi

katika ngazi ya jamii, hasa ambapo mila na desturi zimekita mizizi. Utekelezaji wa programu katika sehemu ambayo kuna desturi za kimila zilizokita mizizi kuhusu jinsia kunahitaji ushiriki mpana wa jamii na utekelezaji endelevu ili kuleta mabadiliko chanya ya kitamaduni.

## Mapendekezo ya utafiti

*Kutumia* mradi huu kufanya tathmini katika mazingira tofauti na kuchunguza kujirudia kwa matokeo ya utafiti wetu pamoja na ushawishi wa sababu za kimazingira.

Kuchunguza *athari zinazoendana za Ujana Salama na mawanda yake*, kwa kuwa, utafiti wa sasa ulipima kwa ujumla athari za mpango wa Ujana Salama ikilinganishwa na utoaji fedha taslimu tu, utafiti haukujikita kwenye matokeo ya kipengele kimoja kimoja.

Kubainisha vipengele vya mradi vyenye ufanisi zaidi, na muunganiko mzuri (ikiwa ni pamoja na vipengele mbalimbali vya mpango wa Ujana Salama na mchango wa sababu za kimazingira kwa kufanya *mapitio ya hatua kwa hatua* ya programu mbalimbali za vijana za kisekta zinazoendana.

Kuchunguza *vikwazo vya kielimu na kujifunza* na nafasi ya tamaduni za kijinsia katika kuchagiza fursa za kielimu na ajira.

Kufanya *ufuatiliaji wa muda mrefu* wa sampuli katika utafiti huu (na tafiti kama hii zinazochunguza programu jumuishi zinazolenga vijana) ili kuelewa ikiwa hatua hizi zinazolenga vijana zinaendelea kuwanufaisha katika utu uzima, kwenye masuala ya afya, uwezeshaji wa kiuchumi na majadiliano ya ndani ya kaya; na kujua ikiwa kuna athari za vizazi (kwa mfano, vijana/watoto wanaolengwa).

## Mapendekezo ya mradi

Kuhakikisha upatikanaji wa *shule bora za sekondari na/au mafunzo ya ufundi* kwa kutoa vocha za bweni au programu nyingine ambazo zinapunguza gharama.

Kuhakikisha kuwa *mtaala wa mafunzo* ya mpango wa Ujana Salama na mbinu za utekelezaji wake zinajikita katika kuhamasisha elimu na mafunzo, ambayo yanaweza kutoa fursa zaidi na bora kwa vijana kwa muda mrefu, ikilinganishwa na fursa za biashara za haraka. Jitihada hizi zinapaswa kujumuisha uwezeshaji wa mafunzo stadi kwa kuwaunganisha vijana na huduma za ufundi.

Kwa kuwa mpango huu na mingine kama hii ni  jumuishi, ni vyema kuimarisha *uratibu na mifumo ya kisekta*, ikijumuisha uhusiano na huduma za VVU na afya ya uzazi na ujinsia (SRH). Pia ni muhimu kuendelea kuimarisha huduma za kijinsia za utoaji taarifa na kuchukua hatua.

Kuwa na *mtazamo wa kijinsia* katika programu za uwezeshaji wa kiuchumi, ikiwa ni pamoja na kubuni na kutekeleza mipango mipana ya kijinsia ili kuongeza athari za miradi kama vile Ujana Salama. Ushiriki usiofaa wa wasichana katika kazi za nyumbani ni kipengele muhimu cha kuzingatia katika kuandaa programu.

Kuboresha *uratibu kati ya washirika wa maendeleo* na kuunganisha juhudi zao. Hii inaweza kusaidia kushughulikia mahitaji yenye sura pana ya vijana walio katika mazingira magumu na kuleta ufanisi katika matumizi ya rasiliamali

Upembuzi wa mikakati ya kukabiliana na ucheleweshaji wa malipo ya ruzuku kwa Walengwa wa Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini unaonesha kuwa hatua zifuatazo zinapaswa kuchukuliwa: (i) kuboresha *mawasiliano na washiriki* kuhusu sifa zao za ustahiki, kiasi cha malipo, majukumu ya pamoja na mabadiliko yanayotarajiwa katika utekelezaji wa programu; (ii) kuboresha njia za kutatua changamoto  katika nyanja zote za maisha ikiwa ni pamoja na kusaidia kutambua huduma za ziada zinazoshughulikia athari za umaskini wenye sehemu nyingi, ikiwa ni pamoja na kusaidia upatikanaji wa huduma za elimu na afya; (iii) *kufuatilia* kaya zilizoathiriwa na ucheleweshaji wa malipo pamoja na zile ambazo 'zinahitimu' kutoka katika Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini kwa muda mrefu; na (iv) kuimarisha *mfumo wa kushughulikia malalamiko*, Ili washiriki wanafahamu haki yao ya mafao ya kinga ya jamii na wanaelewa jinsi ya kuwasiliana na watekelezaji wa programu wakati matatizo yanapotokea.

Utafiti huu ni wa kwanza kutoa ushahidi juu ya ufanisi wa mpango wa Ujana Salama na mingine ya aina hii inayotoa nyongeza ya ruzuku kwa kaya maskini na unaolenga vijana. *Mpango huu wa Ujana Salama ulitekelezwa ndani ya Mpango wa kinga ya jamii unaoendeshwa na serikali*. Kwa kuwa kwa sasa dunia inakabiliwa na wimbi la kuwa na idadi kubwa zaidi ya vijana[14], ni muhimu sana kuelewa muunganiko wa utoaji ruzuku na uwekezaji ambavyo vinaweza kusababisha mabadiliko chanya kwenda utu uzima ili kupata mustakabali bora kwa vijana wa leo na vizazi vyao.

## Shukrani

Muhtasari huu umeandaliwa na Timu ya Tathmini ya Mpango wa Ujana Salama Tanzania; UNICEF Innocenti – Ofisi ya Kimataifa ya Utafiti na Utabiri – Valeria Groppo, Hassan Kihanzah, Lusajo Kajula, Graca Marwerwe, Rosemarie Mwaipopo, Rosemarie Mwaipopo, Leah Prencipe, Nyasha Tirivayi, Jennifer Waidler na Stephanie Zuilkowski; Chuo Kikuu cha Buffalo – Tia Palermo

(Mtafiti Mwenza) na Sarah Quinones; EDI Global – Johanna Choumert Nkolo (Mtafiti Mwenza), Respichius Mitti (Mtafiti Mwenza), Bhoke Munanka, Sadam Matsawili na Marie Mallet: TASAF: Paul Luchemba na Tumpe Mnyawami Lukongo; TACAIDS – Aroldia Mulokozi; na UNICEF Tanzania – Ulrike Gilbert, Paul Quarles van Ufford, Rikke Le Kirkegaard, Frank Eetaama, Jennifer Matafu, Diego Angemi na Luisa Natali.

Ufadhili wa mradi huu wa majaribio na tathmini husika umetolewa na UNICEF Tanzania kwa hisani ya Wakfu wa Oak. Ufadhili wa ziada kwa ajili ya tathmini hii ulitolewa na Idara ya Maendeleo ya Kimataifa ya Uingereza na Ireland Kaskazini (2017–2019), Shirika la Ushirikiano wa Maendeleo ya Kimataifa la Uswisi (2017–2020) na Ofisi ya Mambo ya Nje, Jumuiya ya Madola na Maendeleo (2020-2023) kama ruzuku kwa UNICEF Innocenti. Ufadhili wa ziada wa kukamilisha utekelezaji wa programu ulitolewa kwa hisani ya Irish Aid Tanzania.

Kwa taarifa zaidi juu ya programu na matokeo ya Awamu ya 4, angalia ripoti kamili: Timu ya Tathmini ya Mpango wa Ujana Salama kwa Vijana Tanzania, Tanzania Adolescent Cash Plus Evaluation Team, A Cash Plus Model for Safe Transitions to a Healthy and Productive Adulthood: Round 4 Impact Evaluation Report, UNICEF Innocenti – Global Office of Research and Foresight, Florence, February 2024.

# Marejeo


1 Timu ya Utafiti wa Tathmini ya Vijana ya Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini Tanzania, Utafiti wa Tathmini ya Athari ya Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini (PSSN) kwa Vijana Tanzania: Ripoti ya Mwisho, Ofisi ya Utafiti ya UNICEF – Innocenti, Florence, 2018, <www.unicef-irc.org/publications/942-.html>, imepakuliwa tarehe 20 Septemba 2023.

2 Tathmini hii inaongezea na kuchangia kwenye Mradi wa Uhawilisho, Mpango wa Utafiti na Ujifunzaji wa Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa, Chuo Kikuu cha North Carolina huko Chapel Hill na UNICEF. Kwa taarifa zaidi, angalia tovuti ya Mradi wa Uhawilisho, katika <https://transfer.cpc.unc.edu>, iliyopakuliwa tarehe 20 Septemba 2023.

3 Timu ya Tathmini ya Mpango wa Ujana Salama kwa Vijana Tanzania, Mpango wa Ujana Salama Unaohusu Mabadiliko Salama kutoka Ujanani hadi Utu Uzima wenye Afya na Ustawi: Ripoti ya Matokeo ya Awali, UNICEF Innocenti – Ofisi ya Kimataifa ya Utafiti na Utabiri, Florence, 2018, <www.unicef-irc.org/publications/943-a-cash-plus-model-for-safe-transitions-to-a-healthy-and-productive-adulthood-baseline.html>, imepakuliwa tarehe 20 Septemba 2023; Timu ya Tathmini ya Mpango wa Ujana Salama kwa Vijana Tanzania, Mpango wa Ujana Salama unaohusu Mabadiliko Salama kutoka Ujanani hadi Utu Uzima wenye Afya na Ustawi: Ripoti ya Matokeo ya Kati, UNICEF Innocenti – Ofisi ya Kimataifa ya Utafiti na Utabiri, Florence, 2020, <www.unicef-irc.org/publications/1100-cash-plus-model-for-safe-transitions-to-healthy-and-productive-adulthood-midline.html>, imepakuliwa tarehe 20 Septemba 2023; Timu ya Tathmini ya Mpango wa Ujana Salama kwa Vijana Tanzania, Mpango wa Ujana Salama unaohusu Mabadiliko Salama kutoka Ujanani hadi Utu Uzima wenye Afya na Ustawi: Ripoti ya Matokeo ya Awamu ya 3, UNICEF Innocenti – Ofisi ya Kimataifa ya Utafiti na Utabiri, Florence, 2020, <www.unicef-irc.org/publications/1187-a-cash-plus-model-for-safe-transitions-to-a-healthy-and-productive-adulthood-round-3-report.html>, imepakuliwa tarehe 20 Septemba 2023.

4 Sen, Amartya, 'Maendeleo kama Upanuzi wa Uwezo', katika *Maendeleo ya Jamii (Kitabu cha Darasani)*, iliyohaririwa na James DeFilippis na Susan Saegert, Routledge, n.p., 1990, uk. 319–327. Angalia pia Jinsia na Ujana: Ushahidi wa Kidunia, *Jinsia na Ujana: Kwa nini ni muhimu kuelewa uwezo wa vijana, mikakati ya mabadiliko na mazingira husika?*, GAGE Consortium, n.p., Julai 2017, <www.gage.odi.org/wp-content/uploads/2019/01/Gender-and-Adolescence-CF-FINAL-1.pdf>, imepakuliwa tarehe 20 Septemba 2023.

5 Devereux, Stephen na Rachel Sabates-Wheeler, 'Ulinzi wa Kijamii wa Kimageuzi', IDS Chapisho la Kuanzia 232, Taasisi ya Taaluma za Maendeleo, Brighton, Uingereza, Oktoba 2004, <www.ids.ac.uk/download.php?file=files/dmfile/Wp232.pdf>, imepakuliwa tarehe 20 Septemba 2023.

6 Mfuko wa Watoto wa Umoja wa Mataifa, 'Kinga ya Jamii Unaojali Umri na Jinsia: Mfumo dhana', Chapisho la Kuanzia la Innocenti Na. WP-2020-10, Ofisi ya Utafiti ya UNICEF – Innocenti, Florence, Oktoba 2020, <www.unicef-irc.org/publications/1116- gender-responsive-age-sensitive-social-protection-a-conceptual-framework.html>, imepakuliwa tarehe 19 Septemba 2023.

7 Kwa madhumuni ya kiutawala, TASAF inahusika katika maeneo ya kijiografia ya utekelezaji wa programu kama Mamlaka ya Maeneo ya Utekelezaji ya mradi. Katika Tanzania bara, haya ni sawa na mabaraza ya serikali za mitaa. Katika maeneo ya kiutawala kuna kata na, ndani ya kata, kuna vijiji au mtaa (mtaa ni kitengo cha utawala katika maeneo ya mijini, sawa na kijiji katika maeneo ya vijijini).

8 Upangaji ulifanyika mnamo 2017, baada ya utekelezaji wa awali, na ulitengwa na maeneo ya kiutawala yenye ukubwa wa kijiji (vijiji vikubwa dhidi ya vidogo).

9 Mpango wa Ujana Salama: Ripoti ya Utafiti wa Awali.

10 Asilimia ya vijana waliopotea kwenye ufuatiliaji ilikuwa sawa katika vijiji vya majaribio na ulinganifu. Tabia/sifa za hatua za awali zilibaki kuwa sawa kwenye hatua mbili za utafiti katika jopo la sampuli (yaani, wale waliohojiwa kwenye hatua za awali na katika Awamu ya 4).

11 Tulitumia uchanganuzi wa vipimo vya tofauti-tofauti (ANCOVA), ambapo tulidhibiti thamani ya msingi ya matokeo yanayozingatiwa.

12 Mpango wa Ujana Salama: Ripoti ya Matokeo ya Kati

13 Kimsingi, wasichana walikuwa na uwezekano mkubwa kuliko wavulana kuwa katika shule ya sekondari. Pia walikuwa na kiwango cha juu cha ushiriki katika mafunzo ya Mpango wa Ujana Salama. Sababu hizi, pamoja na mlengo wa mafunzo wa kibiashara na hali nyingine za kimazingira, zilichangia matokeo yaliyobainishwa. Kwa maelezo zaidi, angalia Timu ya Tathmini ya Fedha ya Vijana Tanzania, 'Ujana Salama: Mfano wa Fedha Zaidi juu ya Ustawi wa Vijana na Mabadiliko Salama, Afya – Matokeo ya Awamu ya 3', Muhtasari wa Utafiti wa Innocenti, Na. 2020-23, Ofisi ya Utafiti ya UNICEF – Innocenti, Florence, 2021 , <www.unicef-irc.org/publications/1189-ujana-salama-cash-plus-model-on-youth-well-being- and-safe-healthy-transitions-round-3-findings.html>, ilipakuliwa tarehe 20 Septemba 2023.

14 Idadi ya vijana wenye umri wa miaka 10 hadi 19 ilifikia bilioni 1.3 mwaka 2023, idadi kubwa kuliko hapo awali. Chanzo: Viashiria vya Maendeleo ya Benki ya Dunia (makadirio ya wafanyakazi wa Benki ya Dunia kwa kutumia jumla ya idadi ya watu na mgawanyo wa umri/jinsia wa Idara ya Idadi ya Watu ya Umoja wa Mataifa Matarajio ya Idadi ya Watu Duniani: Mapitio ya 2022). Takwimu zilizopatikana mnamo Oktoba 2023.

**UNICEF** inafanya kazi katika maeneo hatari zaidi duniani ili kuwafikia watoto na vijana wasiojiweza na kulinda haki za kila mtoto, kila mahali. Katika nchi na maeneo 190, tunafanya chochote kinachohitajika ili kuwasaidia watoto kuishi, kustawi na kuonesha uwezo wao, tangu utotoni hadi ujanani. Na hatuachi kamwe.

**UNICEF Innocenti – Ofisi ya Kimataifa ya Utafiti na Utabiri** inashughulikia masuala ya sasa na yanayoibuka yenye umuhimu mkubwa kwa watoto. Huchochea mabadiliko kupitia utafiti na utabiri kuhusu masuala anwai yakiwemo afya ya uzazi na ujinsia haki za watoto, na kuchochea mijadala duniani na kuwashirikisha vijana kikamilifu katika kazi yake.

UNICEF Innocenti inawapa viongozi na wafanya maamuzi ushahidi wanaohitaji ili kujenga ulimwengu bora na salama kwa watoto. Ofisi inafanya utafiti juu ya masuala ambayo hayajatatuliwa na kuibuka, ikitumia data za msingi na sekondari ambazo zinawakilisha sauti za watoto na familia husika. Inatumia mtazamo wa mbele kuweka ajenda za watoto, ikiwa ni pamoja na upembuzi wenye upeo wa mbali, uchambuzi wa mwenendo na kubashiri mwelekeo. Ofisi inazalisha machapisho mbalimbali na ripoti mahiri za kiwango cha juu, inafanya uchambuzi wa sera, na ni jukwaa la mijadala na utetezi kuhusu masuala mbalimbali ya haki za mtoto.

UNICEF Innocenti hutoa majibu ya changamoto inayomsibu kila mtoto.

**Kimechapishwa na**
**UNICEF Innocenti – Ofisi ya Kimataifa ya Utafiti na Utabiri**
Kupitia degli Alfani 58
Florence, Italia

Simu: (+39) 055 20 330
Barua pepe: innocenti@unicef.org
Mitandao ya kijamii: @UNICEFInnocenti on Facebook, Instagram, LinkedIn, Twitter and YouTube

**Nukuu inayopendekezwa:**
Timu ya Tathmini ya Mpango wa Ujana Salama kwa Vijana Tanzania: Mpango wa Ujana Salama Unaohusu Mabadiliko Salama kutoka Ujanani hadi Utu Uzima wenye Afya na Ustawi: Matokeo ya Awamu ya 4', UNICEF Innocenti – Ofisi ya Kimataifa ya Utafiti na Utabiri, Florence, Aprili 2024

© Shirika la Umoja wa Mataifa la Watoto (UNICEF), Aprili 2024

unicef
for every child